# Mbegu ya dhahabu



# Kuna fursa lukuki ufugaji samaki

Louis Kolumbia, Mwananchi
lkolumbia@tz.mwananchipappers.com



**700,000**
**Tani za samaki zinazohitajika kwa mwaka nchini. Kwa sasa tani zinazopatikana ni 500,000**

**02**
**Wastani wa kilo za samaki wanaovuliwa na wavuvi wadogo Zanzibar**

Kushuka kwa kiasi cha samaki wanaovuliwa duniani kumefanya ufugaji uwe ndio mbadala wa ufungufu wa bidhaa hiyo.

Mbali na kuziba pengo la upungufu wa samaki, sekta hiyo ina fursa nyingi ambazo hazijatumiwa ipasavyo kuwanufaisha Watanzania kuboresha kipato chao na cha Taifa kwa jumla.

Licha ya wafugaji kupata manufaa ya kiuchumi, fursa nyingine zinazopatikana kwenye sekta hiyo ni kuzalisha vifaranga, chakula cha samaki, kilimo cha mbogamboga na ufugaji wa ndege wakiwamo kuku na bata.

Samaki kutoka maji chumvi (baharini) na maji baridi (mito na maziwa) wameendelea kutokidhi mahitaji duniani kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, uvuvi haramu, matumizi ya zana zisizofaa za uvuvi na mabadiliko ya tabia nchi.

Tanzania inahitaji tani 700,000 za samaki kwa mwaka ikilinganishwa na tani 500,000 zinazozalishwa na hivyo kusababisha pengo la tani 200,000.

Ripoti ya wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2020/21, inaonyesha kuwa tani 473,592 za samaki zilizalishwa kutokana na uvuvi maji chumvi na maji baridi.

Kiasi hicho cha samaki kiliingiza Sh2.38 trilioni mwaka 2020 sawa na Dola za Marekani Sh1.03.

Ufugaji wa samaki ulichangia tani 18.717 za samaki waliovuliwa mwaka jana wenye thamani ya Dola 642,820.18 sawa na asilimia 3.95, kwa mujibu wa ripoti hiyo.

Ripoti hiyo inasema kuwa mchango wa samaki wa kufugwa katika kiwango cha samaki wanaovuliwa nchini kiliongezeka kutoka tani 220 mwaka 2,000 hadi tani 18,717 mwaka jana, hali inayodhihirisha kwa idadi ya watu wanaojihusisha na kazi hiyo.

Hata hivyo, akiwasilisha bajeti yake ya mwaka wa 2021/22, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema tani 22,793.2 zilizalishwa kufikia Aprili 2021.

"Idadi hiyo inayojumuisha tani 20,258 za samaki, tani 97 za kambamiti, kilo 115 za majongoo bahari na tani 2,438 za mwani," anasema.

## Fursa kwa Watanzania

Hata hivyo, mtafiti mbobevu kutoka Kituo Cha Utafiti bidhaa za Samaki (Tafiri), Dk Amon Shoko anasema ufugaji wa samaki una fursa nyingi kwa Watanzania.

"Watanzania watanufaika zaidi na shughuli jumuishi kama kilimo cha mbogamboga, na ufugaji wa ndege wakiwemo kuku na bata wanaosaidia kuchagiza ufugaji mwanana wa samaki," alisema.

Pamoja na taarifa ya waziri kuwa zaidi ya vifaranga milioni 20 walizalishwa nchini kufikia Aprili 2021, Dk Shoko anasema eneo hilo bado lina fursa kubwa ambazo hazijatumika ipasavyo kuwanufaisha Watanzania. "Watanzania wakinunua vifaa vya kutotolea vifaranga vya samaki na kujikita katika shughuli hiyo watapata manufaa makubwa kiuchumi," alisema.

Dk Shoko alisema Watanzania wanaweza pia kuwekeza kwenye uzalishaji wa chakula cha samaki na kutengeneza fedha nyingi kwa kuwa sehemu kubwa ya chakula hicho inaagizwa kutoka nje ya nchi.

"Si tu kwamba chakula cha samaki kinaagizwa kutoka nje, bali kinauzwa kwa bei kubwa ingawa kuna baadhi ya Watanzania wameanza kunufaika na fursa zinazopatikana kwenye eneo hilo," alisema.

Alisema watu wanaojihusisha na ufugaji wa samaki wanaweza kulima mbogamboga na kufuga ndege kama kuku na bata katika ufugaji jumuishi na kunufaika kiuchumi.

Anasema kinyesi kinachotokana na mifugo hiyo kinaweza kutumika kama chakula kwa samaki.

Kwa kawaida unapofuga samaki sambamba na mifugo mingine jamii ya ndege na mazao ya bustani, mkulima anajihakikishia zaidi fursa za kiuchumi.

# ...huu ndio ufugaji wa kisasa wa samaki

Kujikita kwenye ufugaji wa samaki kunaweza kufanywa kwa kutumia mabwawa, vizimba na keji.

Hata hivyo, mfugaji anatakiwa kufuata maelekezo kadhaa ya kitaalamu ikiwemo kuchagua ardhi sahihi, eneo liwe na maji ya kutosha, maandalizi sahihi ya bwawa, uchaguzi sahihi wa mbegu (vifaranga) na kufuata taratibu za kitaalamu katika kuchanganya aina za samaki.

Vitu vingine vya kuzingatia ni pamoja na kuwapa samaki malisho sahihi na utunzaji wa mabwawa kwa ujumla, kuzingatia ubora wa maji, usalama wa samaki na uvunaji wa kiuchumi.

## Uchaguzi sahihi wa ardhi, ujenzi wa bwawa

Dk Shoko anasema ardhi kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la samaki unatakiwa uwe na kiwango kikubwa cha utunzaji wa maji.

"Ardhi inayofaa inaweza kupimwa kwa kuchimba shimo lenye urefu wa mita moja, kujaza maji na kufunika kuzuia yasipotee kwa kunyonywa na jua na kuyaacha kwa saa 12. Endapo kiasi cha maji hakitapungua baada ya muda huo ardhi hiyo inafaa kwa kuchimba bwawa la samaki," alisema na kuongeza.

"Pia ardhi inaweza kupimwa kwa kutengeneza tonge na kulirusha. Endapo litatua pasipo kusambaratika basi eneo hilo linafaa kwa uchimaji wa bwawa la kufugia samaki."

## Upatikanaji wa maji

Dk Shoko alisema eneo linalotarajiwa kuchimbwa bwawa linapaswa kuwa na kiasi cha kutosha cha maji yatakayotumika kulingana na mahitaji.

## Uchimbaji wa bwawa

Mtaalamu huyo alisema mfugaji anapaswa kupata ushauri wa wataalamu wa samaki katika uchimbaji wa bwawa na kuonya kuwa shughuli hiyo haipaswi kufanywa kiholela.

## Uchaguzi wa vifaranga

Alisema sato na kambale ndizo aina ya samaki zinazotumika katika ufugaji.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, aina hizo za samaki zinaweza kuchanganywa kwenye bwawa moja au kufugwa kila aina peke yake kulingana na maelekezo ya wataalamu.

"Kitu muhimu kwa mfugaji kuzingatia ni mahala atapata vifaranga na utaalamu kabla ya kujikita katika ufugaji wa samaki," anasema.

Anasema ingawa kambale ana tabia ya kula samaki wengine, wanaweza kuchanganywa na sato kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu.

Anashauri mfugaji kutofikiria kufuga samaki kwa muda mrefu ili aingize sokoni samaki wakubwa bali aangalie mahitaji ya soko.

"Ufugaji wa samaki ufanywe kutokana na mahitaji ya soko. Mkulima akivuna mara nyingi kwa mwaka ndivyo atakavtonufaika kiuchumi," ansema.

Dk Shoko anaishauri Serikali kuboresha sera zake na kuondoa vikwazo vinavyokwaza wananchi kujikita katika ufugaji wa samaki.

Anawataka wananchi kutumia wataalamu wa ufugaji samaki wanaotambuliwa na serikali, hatua ambayo itasaidia kuondoa vishoka wanaotoa ushauri potofu kwa wafugaji.

Scanned with CamScanner

na serikali.

Alitoa kauli hiyo juzi Sum-

hospitali zetu za mkoa na halmashauri ambapo lengo

HABARI LEO UK 20

# Asema huduma za ugani ni kiungo kwa watafiti, wakulima

Na Mwandishi Maalumu

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema huduma za ugani ni kiungo muhimu katika kuwasaidia watafiti, wakulima, wafugaji na wavuvi kufanya uzalishaji wenye tija.

Ulega aliyasema hayo wakati alipokuwa akifungua Mkutano wa Mwaka wa Chama cha Wagani Tanzania (TSAEE) uliofanyika jijini Dodoma Desemba 1 hadi 2, mwaka huu.

"Ni muhimu kwenu maofisa ugani kujenga ushirikiano na wakulima, wafugaji na wavuvi ambao utalenga kuwapa taarifa sahihi, kutumia huduma za ugani kama nyenzo ya kusambaza teknolojia, kuelimisha, kutoa ushauri wa kitaalamu na kupata mrejesho wa matumizi ya teknolojia," alisema Ulega.

Alisema katika juhudi za kusaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa maofsa ugani, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) imeandaa mfumo wa kielektroniki unaofahamika 'Huduma za Ugani Kiganjani' kwa ajili ya kuratibu utoaji wa huduma za Ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

"Kwa kutumia mfumo huu, changamoto ya uhaba wa maofisa ugani itapungua lakini pia ufanisi wa utoaji huduma za ugani utaongezeka," alifafanua.

Aliongeza kwamba serikali kupitia taasisi zake za utafiti imeendelea kuibua teknolojia mbalimbali zinazolenga kuongeza na kuboresha uzalishaji wa tija na wa kibiashara katika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

"Iwapo teknolojia hizi zitatumiwa kikamilifu zitaongeza uzalishaji na tija, hivyo kuna umuhimu wa maofisa ugani kutoa zaidi elimu. Mafunzo na hamasa kwa wananchi na wadau wote ili kuongeza matumizi ya teknolojia hizi," alisisitiza.

Aidha, alisema ili kuhakikisha maofisa ugani wanawafikia wafugaji na kutoa ushauri kwa ufanisi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia sekta ya mifugo imenunua pikipiki 300 na sekta ya uvuvi ipo katika mchakato wa kununua pikipiki 10.

Mwenyekiti wa TSAEE, Profesa Catherine Msuya alisema pamoja na mipango mizuri waliyonayo ya kuendeleza chama hicho bado wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kifedha, jambo ambalo linafanya chama kushindwa kuendesha shughuli zake kama inavyotakiwa.

Wa You hiyo juzi

# Wasan milion

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA lisilo la kiserikali, T-MARC Tanzania ambalo ni mshirika wa karibu wa serikali katika mapambano ya vita dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi, limesema katika kipindi cha miaka mitano limeuza na kusambaza kondomu milioni 60 nchini.

Shirika hilo pia limetumia maonesho ya wiki ya Ukimwi kuikumbusha jamii umuhimu wa kupambana dhidi ya maambukizi mapya ya Virusi vinavyosababisha Ugonjwa wa Ukimwi (VVU) na kuendelea kusambaza kondomu.

Maonesho hayo yalifanyika Uwanja wa Ruandansovwe, jijini Mbeya juzi

na ya am Mb ilish ban maa ban kivu amb hiri dhid uzaz uzaz suala W hama kwa maen M wa T- Olive wame

Scanned with CamScanner